

**(NBAA)**  
**BODI YA WAHASIBU NA WAKAGUZI WA HESABU**  
**TANZANIA**



**TAARIFA KWA UMMA**

**KUFANYA KAZI ZA UHASIBU AU UKAGUZI WA HESABU BILA  
KUSAJILIWA NA BODI**

Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) inapenda kuutaarifu Umma ya kwamba hivi sasa wamejitokeza watu wasio kuwa wahasibu au wakaguzi wa hesabu kujihusisha na utayarishaji au ukaguzi wa hesabu za wateja. Kwa mujibu wa sheria iliyounda Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Sura 286 ni makosa kwa yeyote kumwajiri mtu kama mhasibu au mkaguzi wa hesabu ambaye hajasajiliwa na Bodi. Vile vile ni makosa kwa mtu kuajiriwa kama mhasibu au mkaguzi wa hesabu bila kuwa amesajiliwa na Bodi.

Kwa tangazo hii tunaomba kuufahamisha Umma kwamba;

- (1) Kazi za uhasibu au ukaguzi wa hesabu zinafanywa na mtu ambaye amesajiliwa na Bodi kwa mujibu wa sheria na si vinginevyo. Kama ni kampuni ya wakaguzi wa hesabu ni lazima pia iwe imesajiliwa na Bodi.
- (2) Mtu, kampuni au taasisi yoyote inayotaka kumwajiri au kumpa mtu au kampuni yoyote kazi ya kutayarisha au kukagua hesabu ijiridhishe kuwa huyo mtu au kampuni imesajiliwa na Bodi.
- (3) Orodha ya wahasibu, wakaguzi wa hesabu na makampuni ya wakaguzi wa hesabu inapatikana kwenye tovuti ya Bodi ambayo ni [www.nbaa.go.tz](http://www.nbaa.go.tz)
- (4) Kama unajua mtu ambaye anafanya kazi za uhasibu au ukaguzi hesabu bila kusajiliwa na Bodi au taasisi ambayo imeajiri mtu asiyesajiliwa na Bodi, tunaomba utuarifu ili Bodi ifuatilie kwa anwani iliyotajwa hapo chini, sio lazima ujitambulishe jina au anwani yako isipokuwa utoe maelezo ya kutosheleza kumfikia huyo mtu au taasisi iliyotajwa.
- (5) **UMMA UNAOMBWA KUZINGATIA TANGAZO HILI. ENDAPO MTU YEYOTE ATAKUWA NA JAMBO LINALOHITAJI UFAPANUZI ZAIDI ASISITE KUWASILIANA NA BODI KWA ANWANI ILIYOTAJWA HAPA CHINI.**

**MKURUGEZI MTENDAJI**  
**BODI YA WAHASIBU NA WAKAGUZI WA HESABU (NBAA)**  
**MHASIBU HOUSE**  
**MTAA WA BIBI TITI MOHAMED**  
**S.L.P 5128**  
**DAR ES SALAAM**  
**SIMU: +255 22 2211890-9**  
**Nakushi: +255 (22) 2151746, Barua pepe: [info@nbaa.go.tz](mailto:info@nbaa.go.tz)**  
**Tovuti: [www.nbaa.go.tz](http://www.nbaa.go.tz)**